
Kanton Bern
Canton de Berne



# Mwafaka kwa shule ya chekechea

## Suaheli

**Impressum**

Herausgeberin und Copyright
Bildungs- und Kulturdirektion
Amt für Kindergarten Volksschule und Beratung
akvb.bkd@be.ch

Illustration
Peter Gärtl, Thun

Auflage 2021
2019.ERZ.1598

## Wanafunzi wanahitaji majukumu ambayo yatawawezesha kukua, mifano ya kuigwa ambao wanaweza kufwata, na jamii ambapo watahisi wakiwa salama.

Prof. Dr. Gerald Hüther

Wazazi wapendwa,
Mtoto wako hivi karibuni ataanza shule ya chekechea. Huu ni muda muhimu sana kwa sababu watoto katika umri huu wanaweza kusoma kwa urahisi na haraka sana. Tungependa kukupatia mwelekeo wa jinsi ya kukuza maendeleo ya mwanao.

Mahusiano ya kihisia ni ya muhimu sana kwa watoto wachanga. Hii ni kweli kwa tamaduni zote na familia. Watoto kwa kawaida wanataka kujifunza vitu vipya na kugundua ulimwengu unaowazunguka. Usalama wa kihisia katika familia unawawezesha kuchukua hatua za kwanza katika ulimwengu.

Watoto wengi washapitia tukio la kucheza kwa makundi. Kwa mfano, wamekuwa wakicheza na ndugu na dada zao, wana wa majirani, au wana wa makundi ya michezo ambayo wanahudhuria; katika hali hizo wanaweza kutambua watu wa kutazamia juu, kwa mfano wanapata kutambua kiongozi mpya wa kundi la michezo. Wanarejea nyumbani na nyuso zilizojaa tabasamu na maswali na mambo mengi ya kuwaeleza wazazi wao.

Mwanao ataketi kwa muda mrefu na watoto wengine katika shule ya chekechea. Hiki kitakuwa kitu kipya na cha kusisimua kwake. Katika kundi, watoto wakati mwingine watahitajika kusubiria muda wao wa kuzungumza. Mwanao wa kiume au kike atatambua kwamba sio kila mtu anafikiria au anahisi sawia na yeye (au wako sawia) na kwamba vitu tofauti ni muhimu kwa watu tofauti.

Watoto katika umri huu husoma kwa kucheza na wana uwezo wa wastani wa kuelewa mahusiano na masharti. Wana wadogo huiga tabia wanazoziona kwa mazingira yao. Tabia na wanavyojibeba wazazi wao na watu wazima wengine wakuigwa ni vya muhimu sana. Kwa kuweka mfano mwema kwa mwanao kiume au kike, kwa kuwapa nafasi ya wengine wamalize wanachokisema, utakuuza nguvu za mwanao za kusikiza na kuwa makini.

# Kutangamana kwao wenyewe na wengine.

Umgang mit sich und anderen

**Mwanao anataka kutangamana na wenzake**
Jinsi ya kuafikia makubaliano, kuonyesha uamuzi, kupata njia yao, kusubiri: haya ndio mambo watoto wanapaswa kujifunza ili kupata mwelekeo wao katika kundi. Katika kundi la mchezo au katika kituo cha kutwa cha kuwalinda watoto, mwanao wa kiume au kike atajifunza jinsi ya kutangamana na watoto wengine wenye umri mmoja. Mwache mwanao acheze na watoto wengine kwa viwanja pia, au uwaalike watoto wengine kwenu kucheza.

**Mwanao anataka kuwa mojawapo katika kundi**
Katika kundi kubwa la chekechea mwanao wa kiume au wa kike atapaswa kujifundisha kugawana umakini wa mwalimu na watoto wengine katika kikundi. Wakati mwingine Mwanao atahitajika kupuuza hitaji lake au kusubiri muda wake ufike.

**Mwanao anahitaji kuonyesha hisia zake**
Hiki ni kitu kizuri. Msaidie mwanao kutambua, kuonyesha na kuafikia makubaliano na hisia zake. Unapaswa kumfundisha pia mwanao kwamba kuna mipaka ya jinsi mtu anafaa kuwachukulia watu wengine. Kama jinsi mwanao wa kiume au wa kike angependa kuheshimiwa, yeye anafaa Kujifunza kuwaheshimu watoto wengine na watu wazima pia.




## Uhuru na umahiri

Selbstständigkeit und Vertrauen

**Mwanao anataka kufanya vitu vyake mwenyewe.**
Mpatie mwanao nafasi ya kujaribu vitu na kufanya vitu mwenyewe. Mfano, mpatie mwanao nafasi ya kujivalisha na kujivua nguo mwenyewe. Kuenda msalani mwenyewe ni kitu ambacho mwanao anapaswa kujizoesha, ili yeye mwenyewe aweze kujifanyia bila msaada katika shule ya chekechea. Mpe msaada wakati tu ambao anahitajika sana.

**Mwanao anataka kuwa huru**
Kuwa na uaminifu kwa mwanao. Mpe motisha mwanao ya kujaribu tena iwapo kitu hakija kamilika alivyotarajia kwa mara ya kwanza, na ujumlike kwa furaha yake anapo faulu. Mfano muonyeshe mwano njia rahisi ya kufika chekechea au mpe kazi rahisi kama kuchukua barua kutoka kwenye sanduku la barua au kurejesha viombo kwenye kabati.

**Mwanao anataka kujaribu vitu na anataka majaribio.**
Toa vifaa kama penseli za rangi, karatasi, chaki, guluu, mkanda wa kukwama au makasi kwa mtoto wako kucheza navyo. Kuwaacha watoto watoe usaidizi katika shughuli za nyumba au jikoni-kutayarisha, kukata, kupendua, na kuosha mboga mbichi- pia ni njia za kujifunza ujuzi na kuwapa fursa ya kupata uzoefu.



# Kucheza na kusoma

Spielen und Lernen

**Mwanao anataka kucheza**

Mwanao anataka kupata shauku kuhusu vitu na anataka kuweza kujisahau wakati anapocheza. Wakati anapocheza mwanao atajifunza kumakinika, jinsi ya kupanga kitu na kubaki akifanya jambo hilo kwa muda mrefu. Mpe mwanao uhuru huu. Mpe fursa ya kujaribu na vifaa tofauti ikiwemo na vyombo vya matumizi ya kila siku. Muda ambao wewe na mwanao mnacheza pamoja pia ni wa muhimu sana.

**Mwanao anataka kusoma**

Kujifunza inamaanisha vitu vingine vina matokeo vingine havina, Na uzoefu huu unafaa kufundishwa na kunakiliwa. Mwanao alijifunza kutembea kwa sababu aliendelea kuamka kila alipoanguka. Unaweza ukamsaidia kwa kumpa nguvu mwanao kwa kila anchokifanya, kwa kusifu mafanikio na kumpatia motisha kujaribu vitu vipya.

**Mwanao ana mahitaji**

Ni muhimu kuhitaji. Lakini watoto huwa hawapati kila wanachotaka. Watoto wanapaswa kujifunza subira na kukabiliana na kuvunjika moyo. Mazuio na hasira ni hisia za kawaida. Lakini watu au vitu hazifai kuumia au kuharibika kwa sababu ya hisia hizi. Uwezo wa mwanao kuweka kando mahitaji ya wakati mwingine, yatamwezesha mwanao kuwa na nguvu ya kustahimili.



## Kuwasiliana na kueleweka
Sich verständigen und verstanden werden

**Mwanao anataka kuwasiliana**
Fwatilia kile ambacho mwanao anafanya na anachokipitia na umsikize anachotaka kusema. Zungumza na mvulana ama binti wako kuhusu mambo ya kila siku na umuelezee unachokifanya au kitu ambacho mwanao anakiona

**Mwanao anataka kusikiza**
Tazama vitabu vya picha na mwanao, wasimulie hadithi na muimbe nyimbo pamoja. Kwa njia hii watoto wanahisi ukaribu na pia wanajifunza lugha. Zungumza na mzulana ama binti wako katika lugha yako ya kwanza. Ni rahisi zaidi watoto kujifunza lugha ya pili iwapo wana weledi mzuri wa lugha yao ya kwanza.

**Mwanao anataka kujifunza lugha.**
Watoto wadogo hawawezi kumbuka maneno mapya iwapo wamejifunza tu kwenye vyombo vya umeme. Watoto wanahitaji watu wa karibu nao wanawasiliana nao. Wanajifunza vitu vipya na maneno mapya kwa urahisi iwapo ni mtu wa karibu na wanaweza kuyatumia maneno haya kwa haraka.



# Mazoezi ya kimwili na usingizi.

Bewegung und Schlaf

**Mwanao anataka utendaji**
Mwache mtoto wako apande, ajisawazishe, apige samasolti na acheze mpira. Toka nje na mgundue maumbile na mwanao hata kama kunanyesha.

**Mwanao anahitaji kupata usingizi wa kutosha.**
Ili kuweza kukabiliana na mpangilio wa shule ya chekechea, ni kitu cha maana mwanao kupata usingizi wa muda wa masaa kumi au kumi na mawili bila kusumbuliwa. Kiamsha kinywa cha afya na chenye shibe ndiyo jinsi nzuri ya mwanao kupata nguvu asubuhi.

**Mwanao anataka mila**
Mpangilio wa kujirudia na mila isiyobadilika kwa mfano muda wa kula na wa kulala, unampatia mwanao hisia ya kuwa imara na salama.



Iwapo ungependa kusoma Zaidi, ujumbe zaidi unaweza kupatikana kwa www.be.ch/volksschule

Tunawaombea wewe na mwanao muda mwema katika shule ya awali.

